

HALMASHAURI YA WILAYA YA MASWA
(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)

Telegrams: "MSW"
Telephone: 028 2750271
Fax: 028 2750376
E-mail: ded@maswadc.go.tz



S.L.P. 170,
MASWA,
SIMIYU.

Kumb.Na. MDC / AD /30 /31 /VOL.VII /149

16/07/2022

TANGAZO LA KUITWA KWENYE USAILI


Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Maswa kwa kushirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali (NBS) wanapenda kuwataarifu walioomba nafasi za kazi za muda za Sensa 2022 kwa nafasi za Makarani, Wasimamizi wa Maudhui na Msimamizi wa TEHAMA kuwa Usaili utanyika kuanzia tarehe **19/07/2022** na **20/07/2022**. Aidha Usaili katika nafasi za Makarani na Wasimamizi wa Maudhui utafanyika ngazi ya Kata (kwa kila Kata) na Usaili wa Wasimamizi wa TEHAMA utafanyika ngazi ya Wilaya kama ilivyoainishwa katika Ratiba hapo chini.

Wasailiwa waliokidhi vigezo vya Usaili wanapaswa kuzingatia mambo yafuatayo:

- ❖ Cheti cha Elimu na Taaluma
- ❖ Cheti cha kuzaliwa
- ❖ Kitambulisho cha NIDA au namba ya Nida au kitambulisho kingine chochote
- ❖ Kila msailiwa atajigharamia chakula, usafiri na Malazi
- ❖ Wasailiwa wanatakiwa kufika katika eneo la Usaili saa 1:00 asubuhi
- ❖ Orodha ya majina ya waombaji walioitwa kwenye Usaili imeambatanishwa

NA	NAFASI	ENEO LA USAILI	TAREHE	MUDA
1	Msimamizi wa TEHAMA	UKUMBI MKUBWA WA HALMASHAURI	19.07.2022	1:00 ASUBUHI
2	KARANI	MAKAO MAKUU YA KILA KATA	20.07.2022	1:00 ASUBUHI
3	Msimamizi wa MAUDHUI	MAKAO MAKUU YA KILA KATA	20.07.2022	1:00 ASUBUHI

Tangazo hili limetolewa na;


Vivian M. Christian
KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI WILAYA
MASWA.

Nakala: Mbao zote za Matangazo- **Wilaya ya Maswa**